Uchunguzi Unaofanywa na Adult Protective Services (APS)
Maelezo Muhimu

Adult Protective Services (APS) Investigations Fact Sheet

Idara ya Huduma za Ulinzi kwa Watu Wazima (APS) inachunguza ripoti kwamba unaweza kuwa umemnyanyasa, umemtelekeza, umemdhulumu kifedha, au umempuuza mtu mzima mnyonge. Waraka huu unakutaarifu kuhusu mchakato wa uchunguzi, haki zako, na taarifa nyingine muhimu. Kama sehemu ya uchunguzi huu, APS itapitia rekodi na kuhoji watu kuhusu tuhuma hizi.

Matokeo ya uchunguzi huu yanaweza kuwa na athari kubwa kwako. Tafadhali soma waraka huu kwa umakini.

Mchunguzi aliyekabidhiwa kesi yako ni:
Anaweza kupatikana kupitia:

Haki zangu ni zipi?

- Una haki ya kusindikizwa na mtu mwingine (kama rafiki, mwanasheria, mwakilishi wa chama cha ushirika, mwanafamilia, au mlezi) wakati wa mahojiano.
- Ikiwa Kiingereza si lugha yako ya kwanza, una haki ya mkalimani bila malipo (APS hairuhusiwi kutumia wanafamilia kama wakalimani).
- Una haki ya kutoshiriki mahojiano, kuyasitisha, au kupanga tarehe nyingine ya mahojiano hayo.
- Una haki ya kuwapatia APS nyaraka au mashahidi wanaohusiana na tuhuma hizi.

APS watanitaarifu vipi matokeo ya uchunguzi huu?

- APS wanatoa uamuzi kulingana na ushahidi unaokusanywa na APS wakati wa uchunguzi. Aina za uamuzi ambao APS wanatoa ni:
  - **Imethibitishwa:** Kuna uwezekano mkubwa tukio linalotuhumiwa limetokea
  - **Haijathibitishwa:** Kuna uwezekano mkubwa tukio linalotuhumiwa halikutokea
  - **Hakuna ushahidi wa kutosha:** Imeshindikana kubaini iwapo tukio linalotuhumiwa limetokea au la.
- APS ikigundua kuna uwezekano mkubwa tukio limetokea, APS itakutaarifu kwa barua kupitia huduma rasmi au ya kawaida ya posta.
- APS ikigundua kuna uwezekano mkubwa tukio halikutokea, APS itakutaarifu kwa njia ya mdomo. APS inaweza kukupatia barua ukiomba.
- APS ikishindwa kubaini iwapo tukio limetokea, APS itakutaarifu kwa njia ya mdomo. APS inaweza kukupatia barua ukiomba.
- Ikiwa APS haina anwani yako ya sasa, unaweza kukosa barua na tarehe muhimu za mwisho.

Ugunduzi uliothibitishwa unamaanisha nini?

APS ikiamua kwamba tuhuma za kunyanyasa, kupuuza, kutelekeza, au kudhulumu kifedha “zimethibitishwa”, unaweza kuomba usikilizaji wa shauri ikiwa hukubaliani na ugunduzi huo. Uamuzi wa APS ukiungwa mkono baada ya mchakato wa usikilizaji wa shauri, jina lako litawekwa kwenye masjala.

Kuwa kwenye masjala inamaanisha hutaweza kufanya kazi au kujitolea mahali popote unapoweza kuwa na ukaribu usiodhibitiwa na watu wazima wanyonge au watoto. Kwa sasa hakuna njia ya kuondoa jina lako kwenye masjala.

Naweza kupinga uamuzi wa APS?

- APS ikiamua kwamba tukio linalotuhumiwa **halijathibitishwa** au **halina ushahidi wa kutosha** huhitaji kufanya chochote.
- APS ikiamua kwamba tukio linalotuhumiwa **limethibitishwa** na hukubaliani na uamuzi huo unaweza kuomba usikilizaji wa shauri. Barua ya APS itakuambia jinsi ya kufanya hivyo.

Ili kuomba usikilizaji wa shauri, unatakiwa kufanya hivyo hadi saa 5:00 p.m ya siku ya 30 ya kalenda baada ya tarehe ambayo barua ya notisi ya idara hii ilitumwa au kuwasilishwa binafsi kwako, hatua yoyote itakayofanyika kwanza.

Kwa Maelezo Zaidi

Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu APS mtandaoni kupitia https://www.dshs.wa.gov/altsa/adult-protective-services-aps.